

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

Anwani ya Simu: "ELIMU" DAR ES
SALAAM
SIMU: 2110146/2120403/2120412-21
Fax: 255-51-113271 Elimu Tz
Website: www/moe.go.tz



S.L.P. 9121,
DAR ES SALAAM

Kumb: Na: TTDB/363/450/01/47

Tarehe: 17/12/2007

Makamu Mkuu wa Chuo
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania,
S.L.P. 23409,
DAR ES SALAAM. (Aione Prof. Shemweta)

**KUH: WAJIBU NA MAJUKUMU KWA WALIMU WA MAFUNZO MAALUMU
YA MUDA MFUPI 1,500 WALIOANZA MAFUNZO JANUARI, 2007**

Kumbukumbu ni barua yako Na. OUT/ACAD/FE/113 ya tarehe 13/06/2007 kuhusu shauri lililotajwa hapo juu.

Baada ya kupitia mapendekezo yako na kufanya marekebisho katika baadhi ya vipengele nashauri mgawanyo wa majukumu kati ya Chuo Kikuu Huria, Wizara na walimu wa leseni uwe kama ifuatavyo:

Chuo Kikuu Huria:

- (i) Kuandikisha walimu wa Mafunzo Maalumu ya Muda Mfupi (leseni) kwa kuzingatia vigezo vya Chuo Kikuu Huria. Uandikishaji uridhiwe na pande zote mbili na orodha kuwasilishwa wizarani.
- (ii) Kutangaza orodha ya waliochaguliwa
- (iii) Kuandaa na kusambaza vifaa vya kujifunzia kwa walimu wa leseni.
- (iv) Kuendesha mafunzo ya ana-kwa ana kwa walimu wa leseni.
- (v) Kutoa taarifa ya maendeleo ya taaluma ya walimu wa leseni kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.
- (vi) Kuthibitisha uhalali wa walimu wa leseni waliopo katika programu
- (vii) Kutoa taarifa ya mpango wa kuhitimu kwa kila mwalimu wa leseni katika kipindi kisichozidi miaka mitatu.
- (viii) Kutoa maelezo ya matumizi ya fedha iliyolipwa Chuo Kikuu Huria katika kuendesha mafunzo.

WEMU:

- (i) Kuwasilisha orodha ya majina ya walimu wa leseni Chuo Kikuu Huria ili wenye sifa wafikiwiwe kupata mafunzo kwa misingi ya vigezo vya Chuo Kikuu Huria;

- (ii) Kuhakiki orodha inayowasilishwa na Chuo Kikuu Huria;
- (iii) Kuwasiliana na Chuo Kikuu Huria kuhusu vyuo vitakavyotumika kuendesha mafunzo ya ana-kwa ana;
- (iv) Kugharimia malazi na chakula wakati wa mafunzo ya ana-kwa ana;
- (v) Kugharimia mambo muhimu kama ada (tuition fee), vitabu na stationery ikizingatia gharama kwa mwanachuo;
- (vi) Kugharimia wanachuo wakati wa kufanya mazoezi ya vitendo kwa wale watakaobidi kufanyia nje ya vituo vyao; na
- (vii) Kutoa maelekezo muhimu kwa walimu wa leseni baada ya kushauriana na Wizara ya Elimu ya Juu na Chuo Kikuu Huria.

Walimu wa leseni:

- (i) Kuhudhuria mafunzo ya ana-kwa ana na kuthibitisha kumudu programu yenyewe;
- (ii) Kugharimia kujiandikisha na usafiri kwenda katika vituo vya mafunzo ya ana-kwa ana na mafunzo ya vitendo;
- (iii) Kuonesha kujali, kuheshimu taratibu na maadili ya ualimu wawapo katika vituo vya mafunzo ya ana -kwa ana na mafunzo ya vitendo;
- (iv) Kuthibitisha kuwepo katika vituo walivyopangiwa kufundisha; na
- (v) Kuhakikisha mawasiliano yote yanapitia kwa Mkuu wa Shule ya sekondari anayofundisha.

Maelezo haya hayazuii wahusika kutafuta njia nyingine za kugharimia mafunzo haya ya wizara. Mgawanyo huu wa majukumu unazingatia lengo la kufanikisha programu hii na unarekebisha maelezo na ahadi zilizotolewa awali



.O.P.J. MHAIKI

NAIBU KATIBU MKUU

Nakala: Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.
:
:
:
:
Wakaguzi Wakuu wa Elimu Kanda.
Maafisa Elimu (M)
Wakuu wa Vyuo.